

## MWONGOZO WA UHAMISHAJI WA MAKAZI NA WATU

### Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari

#### Ufafanuzi wa Mradi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, imeandaa mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari nchini utakaofahamika kwa kifupi kama SEQUIP. Madhumuni ya mradi huu ni kuongeza ufikiwaji wa elimu ya sekondari, kuwapatia wasichana mazingira bora ya kujifunza na kuboresha uhitimu bora wa elimu ya sekondari kwa wasichana na wavulana

**Eneo la kwanza (1):** Kuwajengea Wasichana Uwezo Kupitia Elimu ya Sekondari na Stadi za Maisha.

1.1 Kuanzisha shule salama: Utekelezwaji wa shule salama unahusisha: (i) kutoa mafunzao uongozaji wa shule na ushauri kwa walimu; (ii) mafunzo ya stadi za maisha kwa wanafunzi; (iii) huduma za mafunzo ya kanuni za mwenendo na jinsia kwa kutumia mbinu za pedagogical; (iv) kuwajengea walimu wakuu, bodi za shule kuhusu ukatili wa kijinsia na masuala ya shule salama; (v) Kuwepo na mfumo wa ufuatiliaji mashuleni na madarasani kwa ajili ya utambuzi wa awali na kuingilia kati wasichana wali katika hatari ya kuacha shule; na (vi) mfumo wa kijamii kwa ajili ya usalama mashuleni.

1.2 Kukuza uhitimisha wa elimu ya sekondari kwa wasichana kupitia njia mbadala za ubora wa elimu, ikiwa pamoja na:

- a. Kuwepo na mpangilio wa mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kufuatilia uachaji shule kwa wasichana katika ngazi ya taifa na wilaya na kutoa taarifa muhimu kwenye mpango na utekelezaji wa njia mbadala za ubora wa elimu (AEP)
- b. vituo vya njia mbadala za elimu na mamlaka ya serikali za mitaa (LGAs) watafanya shughuli za ufikiwaji wa wasichana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu kwenye jamii ikiwa pamoja na shughuli za kufanyika kwa mikutano ya kijamii ya njia mbadala za elimu, kutoa taarifa kupitia redio na televisheni, mabango na vipeperushi.
- c. kukuza ufikiwaji wa njia mbadala za ubora wa elimu kupitia (i) upanuzi wa mtadao wa vituo njia mbadala za ubora wa elimu; na (ii) kutoa punguzo la ada kwa wasichana wanaoishi katika mazingira magumu
- d. Ubora wa kifurushi cha uimarishaji wa wanafunzi kujifunza njia mbadala za ubora wa elimu pia zitatekelezwa.

**Eneo la Pili (2):** Kufundisha na Kujifunza kwa Ufanishi kwa Kuwezesha Mifumo ya Kidigitali

- a. Ufanisi katika kufundisha na kujifunza
  - i. kifurushi kidogo ambacho kitakuwa na rasilimali muhimu za kufundushia na kujifunza kwenye shule zote: kifurushi hicho kitakuwa na vitabu vya kutosha na muongozo wa mwalimu kwenye masomo muhimu (Kiingereza, Hisabati na Sayansi)
  - ii. Usawa, walimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia watapelekwa mashuleni
  - iii. uendeleaji wa huduma za mafunzo kwa walimu wa sekondari kwenye masomo ya kiingereza, hisabati na sayansi kwa ajili ya kuboresha mafunzo ya darasani kwa vitendo.
  - iv. kutathmini ujifunzaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari ili kutoa nafari ya kurekebisha: kukubali uingiliaji kai wa awali ili kuzuia wanafunzi wa kike kuacha shule kwa ajili ya tatizo la uelewa/kijifunza.
- b. Kuwezesha mfumo wa kidigitali wa kufundishia masomomo ya hisabati, sayansi and kiingereza
  - i. Kuanzisha mfumo wa TEHAMA kwenye mpango na mkakati wa elimu kwa elimu ya sekondari
  - ii. yaliyomo kwenye mfumo wa kidigitali yaunganishwe na fungu la kufundishia masomo ya kiingereza. hisabati na sayansi.

**Eneo la tatu (3):** Kupunguza Vikwazo vya Elimu kwa Wasichana Kupitia Uwezeshaji wa Upatikanaji wa Elimu ya Sekondari

- Kupanua mtandao wa elimu ya sekondari ili kupunguza umbali wa shule za sekondari hasa vijijini. SEQUIP itatoa ufadhili kupitia maradi kwa kuangalia idadi ya namba za shule kwenye kila mamlaka ya serikali za mitaa ili kufikia kiwango cha chini cha miundombinu.
- kutoa msaada ili kuinua shule za sekondari zilizopo kwa kutumia kiwango cha chini cha fungu la miundombinu (idadi ya madarasa/wanafunzi, utoshelezaji wa maji na vifaa vya usafi wa mazingira, maabara za sayansi, umeme n.k.). Lengo ni angalau asilimia 50 ya shule zote zilizopo kwenye mamlaka zote za serikali za mitaa zitaweza kufikia malengo ya chini yaliyowekwa,

**Eneo la Nne (4):** Kutoa Msaada wa kitaalamu, Kufanya Tathmini ya Athari ya Mradi na Uratibu wake.

**Mwongozo wa Mpango wa Uhamishaji wa Makazi na Watu**

Mwongozo huu wa uhamishaji wa makazi na watu umeandaliwa kwa kufuata vipengele muhimu vya Sheria za Tanzania, na Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na Kijamii wa Benki ya Dunia. Vigezo tisa vilivyoainishwa kwatika Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na Kijamii wa Benki ya Dunia vimetumika katika kuandaa mwongozo huu wa uhamishaji wa makazi na watu. Kigezo Na. 5 kinachohusu uchukuaji wa ardhi, katazo la matumizi ya ardhi na Uhamishwaji wa Makazi kwa lazima kinaitaka miradi yote kuepuka kuhamisha watu kwa lazima kwenda kwenye makazi mbadala, kuepuka au kupunguza uhamishwaji wa makazi usio wa hiari na kupunguza athari za kijamii na kiuchumi zitokanazo na utwaaji wa ardhi, na zuio la matumizi ya ardhi. Pamoja na hayo, mradi utatumia sheria husika za nchi zinazohusu utwaaji wa ardhi. Sheria kuu zilizopo ni pamoja na Sheria ya Ardhi Na. 4 (1999) [Sura ya 113 mapitio ya 2002], Sheria ya Ardhi ya Kijiji Na. 5 (1999), [Sura ya 114 mapitio ya 2002], Sheria ya Mahakama ya Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya 2002 [Sura ya 216], Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya 2007, Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya 2007, Sheria ya Upimaji wa Ardhi Na. 32 ya 1957 kama ilivyorekebishwa, Sheria ya Utwaaji wa Ardhi Na. 47 ya 1967, Sheria ya Usajili wa Ardhi Na. 36 ya 1953 kama ilivyo rekebishwa, na Sheria ya Uthamini na Uandikishwaji wa Wathamini Na. 7 ya 2016.

Mradi huo pia umeandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Jamii, Mwongozo wa Makundi yaliyo katika Mazingira Hatarishi na Mwongozo wa Ushirikishwaji wa Wadau ili kuhakikisha kuwa mradi unatekelezwa na kuendelezwa katika ustawi wa kijamii na mazingira, sambamba na Mwongozo wa Masuala ya Kimazingira na Kijamii wa Benki ya Dunia, pamoja na sheria za nchi.

Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari au kwa kifupi SEQUIP unaweza ukapelekea kutwaliwa kwa ardhi / au kuhamishia watu kwenye makazi mbadala bila hiari (kuhamishwa kwa makazi au maeneo ya kufanyia shughuli za kiuchumi) kwa watu katika maeneo ambayo shule mpya zinatarajiwa kujengwa. Maeneo yanayotarajiwa kujengwa shule, aina ya makatazo ya matumizi ya ardhi na watakaoadhirika na ujenzi au makatazo hayo bado hawajajulikana katika hatua hii. Sababu hii ndiyo imepelekea kuandaliwa kwa Mwongozo huu wa Kuhamisha watu na makazi.

### **Madhumuni ya Mwongozo wa Uhamishaji wa Makazi na Watu**

Madhumuni ya Mwongozo wa Uhamishaji wa Makazi na Watu ni:

1. Kuepuka au kupunguza uhamishaji wa makazi bila hiari kwa kubuni mipango mbadala ya miradi ikiwemo kuchagua maeneo ya miradi;
2. Kuepuka utwaaji wa ardhi kwa nguvu;
3. Kupunguza athari zisizoepukika zinazotokana na utwaaji wa ardhi kisheria;

4. Kuboresha maisha ya makundi ya watu walio hatarini au wasio na makazi maalumu kwa kufidia thamani ya ardhi na mali inayotwaliwa; na
5. Kuhakikisha kuwa shughuli za uhamishaji wa makazi na watu zinaratibiwa na kutekelezwa kwa kutoa taarifa sahihi, kufanya majadiliano ya pamoja, pamoja na ushirikishwaji wa wahusika.

Mwongozo wa uhamishaji wa makazi umeweka kanuni za utwaaji wa ardhi pamoja na fidia zake, taratibu za kitaasisi na vigezo vitakavyotumika ili kuzingatia mahitaji ya watu watakao athiriwa na mpango baada ya eneo husika kubainishwa. Baada ya taarifa muhimu kutolewa, mwongozo huu utafafanuliwa kwenye mpango husika wa uhamishaji wa watu na makazi.

### **Vigezo na Stahili za Walioathiriwa**

Kwa kuzingatia masharti ya Kigezo Na. 5 cha Mwongozo wa Masuala ya Kimazingira na Kijamii cha Benki ya Dunia na mchakato wa utekelezaji wa uhamishaji wa makazi, makundi yafuatayo yanastahili kupewa fidia:

- a) Wale wenye umiliki rasmi wa ardhi au thamani (ikiwa ni pamoja na Hati Miliki za Kimila na Umiliki wa Kitamaduni unaotambulika kisheria)
- b) Wale wasiokuwa na umiliki rasmi wa ardhi au thamani (wakati tathmini inafanywa) lakini wanaoushahidi unaotambulika wa umiliki wa ardhi hiyo au thamani husika.
- c) Wale ambao, kisheria, hawana haki ya kumiliki kisheria ardhi walionayo au thamani walizonazo.

Kipengele (a) na (b) hapo juu itawahusu wale wanaotakiwa kupewa fidia kutokana na ardhi itakayochukuliwa, pamoja na misaada mingine kulingana na matakwa ya kisheria. Kipengele (c) hapo juu watapewa msaada wa makazi mbadala kama fidia ya ardhi wanayoishi au kutumia, pamoja na misaada mingine ya kuwawezesha kuishi katika makazi mbadala inapobidi kwa mujibu wa sheria.

Kigezo cha kwanza kitazingatia muda tathmini ilipofanyika. Kama kaya ilikuwa kwenye eneo husika wakati sensa ya makazi inafanyika, mkuu wa kaya atastahili kupewa fidia kulingana na mali watakazopoteza, na kupewa msaada wa makazi mapya kama inahitajika. Kama mtu alivamia eneo la mradi baada ya sensa ya makazi kufanyika, hatopewa fidia.

Kaya zilizoathirika zitastahili fidia zifuatazo kutokana na athari walizopata kwa kuhamishiwa kwenye makazi mbadala kupisha mradi wa kuimarisha ubora wa shule za sekondari. Kama sehemu ya maandalizi binafsi ya kuhamia kwenye makazi mbadala, vigezo na stahili vitahuishwa ili kukidhi gharama halisi za kuhamia kwenye makazi mbadala. Tathmini ya

thamani itafanywa kwa kutumia njia mbalimbali zilizoainishwa katika sheria za Tanzania na pia kwa kuzingatia kanuni za gharama kwa mujibu wa sheria.

Jedwali la Stahiki			
Ardhi na Mali	Athari zilizotokea	Mtu/watu walioathiriwa	Fidia/Stahiki/Faida
Kutwaliwa kwa ardhi ya kilimo na mifugo	Kutwaliwa kwa ardhi iliyokuwa inatumika kwa shughuli za kilimo, au malisho ya mifugo. Ikiwa ni pamoja na sehemu ya ardhi inayobaki ambayo haitoshi kwa matumizi au haikidhi vigezo vya sheria ya mgawanyo wa ardhi	Mmiliki wa Ardhi (mwenye umiliki rasmi au usio rasmi)	<p>Fidia (fedha au mali) inayolingana na thamani halisi bila kuzingatia uchakavu pamoja na gharama za kubadili umiliki. Ardhi inayotolewa kama fidia inatakiwa kuwa na ubora unaolingana na ardhi inayochukuliwa (rutuba, eneo ardhi ilipo, n.k.).</p> <p>Posho ya usumbufu</p> <p>Kurejesha maisha ya wakazi katika hali waliyokuwanayo awali kwa mujibu wa sheria: Hatua sahihi za kuwarejesha wakazi katika maisha yao waliyozoea ni lazima zizingatiwe na zijumuishe msaada wa kuboresha ardhi na kuwa katika hali inayofaa kwa kilimo.</p>
		Wale wasio na umiliki rasmi wa ardhi waliyonayo, au wanayoitumia.	Fidia za kuendeleza ardhi iliyotolewa kama fidia (fedha au thamani) ili kumwezesha aliyepoteza ardhi yake kurudisha maisha yake katika hali

			aliyokuwa nayo awali.
Kutwaliwa kwa ardhi ya makazi	Kutwaliwa kwa ardhi inayotumika kwa makazi. Ikiwa ni pamoja na sehemu ya ardhi inayo baki ambayo haitoshi kwa matumizi au haikidhi vigezo vya sheria ya mgawanyo wa ardhi	Mmiliki wa Ardhi (umiliki rasmi au usio rasmi)	<p>Fidia (pesa au mali kama itakavyochaguliwa na muathirika wa mradi) inayolingana na thamani halisi ya ardhi iliyotwaliwa pamoja na gharama zozote za kuhamisha umiliki wa ardhi. Kama fidia ni ya mali, fidia hiyo ilingane na thamani halisi ya sehemu ardhi ilipo pamoja na hati miliki ya mali husika.</p> <p>Posho ya usumbufu</p> <p>Posho ya usafiri</p>
		Wale wasio na umiliki rasmi wa ardhi wanayomiliki au wanayotumia	<p>Msaada (pesa au mali – eneo la fidia has kwa watu wanaoishi katika mazingira magumu) wa kuhamia kwenye makazi mbadala ili kuwawezesha walioathiriwa kuendelea na maisha yao kwenye makazi mbadala.</p> <p>Fidia za maendeleo yaliyofanywa juu ya ardhi (fedha au mali)</p>

Kutwaliwa kwa ardhi iliyokodishwa	Ardhi inayotumiwa na wapangaji/waliokodi (waliokodi kwa njia zilizo rasmi au zisizo rasmi) kwa ajili ya makazi au shughuli za kiuchumi	Kukodisha/iliyomilikishwa kwa mtu mwingine kwa muda	Marejesho ya kodi yoyote; yaani, kodi iliyolipwa kwa muda ardhi iliyotumika na kodi iliyolipwa kwa matumizi ya ardhi baada ya ardhi kutwaliwa. Fidia ya miezi 3 ya kukodisha ardhi. Msaada wa kupata ardhi nyingine ya kukodi/mali nyingine. Msaada wa kuhamia sehemu nyingine (gharama za usafiri + posho)
Kuathiriwa kwa miundombinu	Sehemu ya miundombinu imeathiriwa na inafaa kuendelea kutumika	Mmiliki wa miundombinu	Fidia ya majengo yaliyoathiriwa pamoja na thamani nyingine zisizohamishika, bila kuzingatia uchakavu. Msaada wa gharama za matengenezo ya miundombinu iliyobakizwa. Haki ya kupata vifaa vya kumudu maisha, ambavyo havitakatwa kwenye fidia itakayotolewa.
		Kukodisha/iliyomilikishwa kwa mtu mwingine kwa muda	Fidia ya mali iliyoathirika (maboresho ya uhakika ya mali ya mkodishaji) bila kuzingatia uchakavu. Fidia ya usumbufu ambayo inalingana na gharama za



			ukodishwaji wa ardhi kwa muda wa miezi miwili.
	Miundombinu yote imeathiriwa na haifai kuendelea kutumika.	Mmiliki	Fidia ya miundombinu yote iliyoathiriwa pamoja na mali zote zisizohamishika bila kujali uchakavu, au kupewa miundombinu mbadala yenye thamani/ukubwa sawa na iliyoathirika katika eneo sahili kama ilivyoshauriwa na Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Makazi na Watu. Kupewa mahitaji ya kujikimu kimaisha bila kukatwa kwenye fidia itakayotolewa. Msaada wa kuhamia kwenye makazi mapya (posho ya umbali atakaosafiri + gharama za usafiri).
		Mpangaji/Mmiliki wa ardhi	Fidia ya mali zitakazoharibika (maendelezo yanayothibitika yaliyofanywa na mpangaji) bila kujali uchakavu. Msaada wa kuhamia kwenye makazi mapya (posho ya umbali atakaosafiri + gharama za usafiri + gharama za malazi,

			<p>kama itakavyohitajika). Msaada wa kupata sehemu nyingine ya kupanga.</p>
	<p>Kuathiriwa kwa sehemu ya miundombinu au miundombinu yote</p>	<p>Makazi holela/makazi yasiyo rasimishwa</p>	<p>Fidia ya miundombinu yote iliyoathiriwa pamoja na mali zote zisizohamishika bila kujali uchakavu. Msaada wa kuhamia kwenye makazi mapya (posho ya umbali atakaosafiri + gharama za usafiri+ gharama za malazi, kama itakavyohitajika) na msaada wa kupata sehemu nyingine ya makazi, inashauriwa zaidi kuwa ni ndani ya eneo la jamii ambayo mradi unaanzishwa. Au, kupata msaada wa makazi katika nyumba ya kupanga au katika mpango wa makazi ya watu (kama yapo).</p>
	<p>Kuathiriwa kwa sehemu ya miundombinu au miundombinu yote</p>	<p><i>Machinga</i> / mmiliki wa biashara (bila leseni ya biashara, duka lililokodishwa)</p>	<p>Fidia inayolingana na mapato ya miezi miwili ambayo italinganishwa na kumbukumbu za ulipaji wa kodi katika kipindi cha mwaka uliopita (au kumbukumbu za</p>

			<p>ulipaji wa kodi kwa biashara inayofanana na hiyo, au kufanyika kwa makadirio), au posho ya kuhamishwa; fidia yoyote itakayokuwa na kiwango kikubwa kati ya hizo tajwa hapo juu itatumika.</p> <p>Gharama za kuhamisha makazi Msaada wa kupata eneo mbadala la kuanzisha biashara.</p>
	<p>Kuathiriwa kwa sehemu ya miundombinu au miundombinu yote</p>	<p>Mmiliki wa biashara (umiliki ulio rasmi)</p>	<p>Fidia ya miundombinu yote iliyoathiriwa pamoja na mali zote zisizohamishika bila kujali uchakavu.</p> <p>Kupewa mahitaji ya kujikimu kimaisha bila kukatwa kwenye fidia itakayotolewa.</p> <p>Fidia inayolingana na mapato ya miezi miwili ambayo italinganishwa na kumbukumbu za ulipaji wa kodi katika kipindi cha mwaka uliopita (au kumbukumbu za ulipaji wa kodi kwa biashara inayofanana na hiyo, au kufanyika kwa makadirio), au posho ya kuhamishwa; fidia yoyote itakayokuwa</p>

			na kiwango kikubwa kati ya hizo tajwa hapo juu itatumika. Gharama za kuhamisha makazi Msaada wa kupata eneo mbadala la kuanzisha biashara
Mazao yaliyoko shambani (yaliyo hai)	Mazao yaliyoathiriwa na utwaaji wa ardhi/ au kutwaliwa kwa muda mfupi au kutumia ardhi ya mmiliki	Mtu aliyeathiriwa na mradi (kama ni mmiliki, mpangaji, au makazi yasiyo rasmi)	Fidia ambayo italingana na wastani wa miaka mitatu wa bei ya soko kwa mazao yaliyokomaa na yakavunwa kama inawezekana, mtu aliyeathiriwa na mradi ataruhusiwa kuvuma mazao (ya muda mfupi au muda mrefu) kabla ya kuhama katika eneo. Msaada wa kimaisha kama unahitajika (msaada wa kupata kazi, mafunzo ya kujengewa ujuzi, kuanzisha shughuli za kilimo)
Miti	Miti itakayotwaliwa pamoja na ardhi	Mtu aliyeathiriwa na mradi (kama ni mmiliki, mpangaji, au makazi yasiyo rasmi)	Fidia ya fedha kulingana na aina, umri, na thamani inayolingana na mazao ya miti iliyoathiriwa, pamoja na fidia ya usumbufu. Msaada wa kimaisha kama unahitajika (msaada wa kupata kazi, mafunzo ya kujengewa ujuzi, kuanzisha shughuli za

			kilimo).
Utwaaji wa ardhi kwa muda	Utwaaji wa ardhi kwa muda	Mtu aliyeathiriwa na mradi (kama ni mmiliki, mpangaji, au makazi yasiyo rasmi)	Fidia ya fedha kwa hasara yoyote ya mapato. Fidia ya fedha kwa ajili ya ardhi iliyotwaliwa kwa muda (gharama za kukodi).
Biashara za kuhamahama	Biashara, maegesho ya taksi, baisikeli	Mmiliki wa biashara, wafanyakazi	Sehemu mbadala ya kuendelea na biashara itabainishwa, gharama za usafiri kama zinahitajika, fidia ya mali zilizoathiriwa kama inatakiwa, kuathiriwa kwa biashara (miezi 3) kama itatakiwa. Posho ya usafiri + posho ya umbali atakaosafiri.
Kupoteza mapato	Kupoteza faida/mapato kwa sababu biashara imeathiriwa na kutwaliwa kwa ardhi	Mmiliki wa biashara	Faida kamili ya miezi mitatu ya biashara iliyoathiriwa kama itakavyo thibitishwa na mkaguzi wa mahesabu, pale ushahidi utakapothibitisha, faida hiyo itazidishwa mara miezi 36. Kwa biashara zisizo rasmi ambazo hazijafanyiwa ukaguzi wa mahesabu, makadirio au fidia za athari za makazi zitatumika kutoa fidia (kuamuliwa hatua

			kwa hatua).
--	--	--	-------------

## **Ushirikishwaji wa Wadau**

Pale ambapo ardhi itahitajika kutwaliwa kwa matumizi ya mradi, kutakuwa na majadiliano na ushirikishwaji wa wanajamii husika na watu mbaao ardhi yao itachukuliwa. Watu watakaoathiriwa na mradi huo watataarifiwa kuhusu matumizi yaliyokusudiwa na mradi katika ardhi husika, huduma na miundombinu itakayojengwa. Watu watakaoathiriwa na mradi watataarifiwa kuhusu:

- Haki zao na uchaguzi wao kuhusu fidia na makazi mapya;
- Fursa za kitaalamu na kiuchumi pamoja na njia mbadala zitakazopatikana kwenye makazi mapya;
- Mchakato na tarehe zilizopangwa za kutoa fidia na kuhamia kwenye makazi mapya;
- Viwango vya fidia halisi za gharama na mali; na
- Mapendekezo ya hatua na gharama za kumudu na kuboresha maisha.

Mbinu na michakato itakayotumika itategemea hali halisi pamoja na jambo husika linaloshughulikiwa pamoja na eneo ambalo wahanga watahamishiwa. Ripoti za Mpango wa Uhamishaji Makazi na Watu zitatolewa katika ngazi ya kijiji kupitia mikutano ya hadhara ya vijiji na mamlaka husika za serikali za mitaa. Mradi hautaidhinisha ujenzi mahali ambapo utalazimisha watu kuhamia kwa nguvu au kuchukua ardhi kwa nguvu.

Aidha, njia za kupokea na kushughulikia malalamiko zitaanzishwa; zitakuwa za wazi na zisizo na upendeleo na zitazingatia vigezo vya mazingira na jamii. Utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko utafanya kazi kwa kupitia Kamati za Ujenzi wa Shule ambazo zitaanzishwa katika kila shule na mabaraza ya vijiji. Malalamiko ambayo hayataweza kushughulikiwa katika ngazi hii yatafikishwa katika ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa na ngazi ya mkoa kama itakavyohitajika.

## **Uandaaji na Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Makazi na Watu**

Uhitaji wa Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Makazi na Watu utabainishwa wakati wa kutathmini sehemu ya kuanzisha mradi uliopendekezwa. Baada ya kubainisha athari za kuhamisha makazi na watu wakati wa tathmini, kitu cha kwanza ni kubainisha kama kuna eneo mbadala ambalo litaepusha kuhamisha wakazi wengine au litahamisha wakazi wachache sana. Pale ambapo hili litashindikana, basi kutakuwa na uhitaji wa Mpango Kazi wa Kuhamisha Makazi na Watu.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawajibika kuandaa Mpango Kazi wa Kuhamisha Makazi na Watu. Mbinu ya ushirikishwaji itatumika kukamilisha zoezi hili. Hii ni njia bora ya kukamilishia Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Makazi na Watu utakaokubalika na kutatua

malalamiko yahasuyo mpango huo. Baada ya Mpango Kazi huo kukamilika, utawasilishwa kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia/Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha unaendana na Mwongozo wa Uhamishaji wa Makazi na Watu. Baada ya hapo, Mpango Kazi utawasilishwa Benki ya Dunia ili kupata kibali kabla ya kuanza utekelezaji wake. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaongoza utekelezaji wa Mpango Kazi, na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia/Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itafuatilia ili kujua kama utekelezaji wa shughuli unaendana na mahitaji ya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Makazi na Watu.

Vipengele muhimu vya Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Makazi na Watu, kama vilivyoanishwa katika Kigezo Na. 5 cha Mwongozo wa Masuala ya Kimazingira na Kijamii ni kama ifuatavyo (vipengele vingine vinaweza kuongezwa):

- Maelezo ya mradi;
- Madhumuni ya mpango wa makazi mbadala;
- Kubainisha madhara yatakayosababishwa na mradi na watu watakaoathiriwa na mradi;
- Sensa ya taarifa za uchumi na kijamii za watu watakaoathiriwa na mradi, ikiwa ni pamoja na taarifa ya makundi ya watu walio katika hatari;
- Mwongozo wa kisheria wa utwaaji wa ardhi na fidia zake;
- Vigezo vya fidia kwa mtu alieathiriwa na misaada mingine ya kuishi kwenye makazi mbadala;
- Tathmini na muongozo wa ulipaji wa fidia;
- Maelezo ya msaada wa kuanzisha makazi mbadala na uanzishaji wa shughuli za kumudu gharama za maisha;
- Bajeti ya kina;
- Utaratibu wa utekelezaji;
- Maelezo ya majukumu ya taasisi (mwongozo wa taasisi husika);
- Muongozo wa majadiliano na wanajamii (uma), ushirikishaji, na mpango wa maendeleo;
- Maelezo ya vifungu vitakavyotumika kushughulikia malalamiko; na
- Muongozo wa ufuatiliaji, kufanya tathmini, na kutoa ripoti.



## **Ufuatiliaji na Tathmini**

Mpango wa ufuatiliaji unahitajika ili kutathmini kama malengo ya uanzishaji wa makazi mbadala na utoaji wa fidia yamefanikiwa. Mpango huo wa ufuatiliaji utabainisha vipengele vya kufuatilia, muda wa ufuatiliaji na kutoa rasilimali za ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na wahusika au taasisi zitakayofanya shughuli za ufuatiliaji. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itafuatilia na kufanya tathmini za utekelezaji wa Mpango wa Uhamishaji wa Makazi na Watu kwa robo au nusu ya muda wa utekelezaji wa mpango wa uhamishaji wa watu (kulingana na hali ilivyo).

## **Uwasilishaji wa Maoni Kuhusu Rasimu ya Mwongozo wa Uhamishaji Makazi na Watu**

Maoni kuhusu rasimu yanaweza kutolewa kwa kupitia njia zifuatazo:

### **Vikao:**

<b>Mkoa</b>	<b>Halmashauri</b>	<b>Ukumbi</b>	<b>Tarehe</b>
Singida	Singida Manispaa	Halmashauri	26 Agosti 2019
Manyara	Babati Mji	Halmashauri	27 Agosti 2019
Manyara (VG)	Mbulu Vijijini	Yaeda chini	28 Agosti 2019
Pwani	Kibaha Mji	Halmashauri	30 Agosti 2019

**Barua pepe:** [tabitha.etutu@moe.go.tz](mailto:tabitha.etutu@moe.go.tz), [tulinagwe.ngonile@tamisemi.go.tz](mailto:tulinagwe.ngonile@tamisemi.go.tz)

**Simu / Ujumbe wa simu:** +255716626631, +255713567280

**Tovuti:** [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz), [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz)